(3) Iwapo taarifa inatumika katika mwenendo wa mahakama, mbali na uchunguzi, mahakama inaweza, kumuulta na kumuuliza maswali Mkemia Mkuu wa Serikali au Mchunguzi wa Kimaabara wa Serikali juu ya usahihi wa taarifa hiyo.

Shahidi
mtaalamu

19. Taarifa iliyotolewa na Mchunguzi wa Kimaabara wa Serikali itakubalika na itatumika kama ushahidi wa taarifa au mambo yaliyomo katika ripoti isipokuwa kama upande mwingine unahitaji Mkemia Mkuu wa Serikali au Mchunguzi wa Kimaabara wa Serikali ambaye ameandaa ripoti hiyo kuitwa kama shahidi.

SEHEMU YA TANO
HUDUMA ZA WAKALA
(a) Huduma za Sayansi Jinai na Vinasaba

The Government Chemist Laboratory Authority Act

-
- Huduma za maabara ya sayansi jinai
- 20.**-(1) Itakuwepo ndani ya Mamlaka, maabara itakayoshughulikia masuala ya huduma za sayansi jinai na Vinasaba.
(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Mamlaka itafanya uchunguzi wa sayansi jinai ya-.
(a) toksikolojia;
(b) jinai, kemia na dawa za kulevyta; na
(c) bailojia na vinasaba vya binadamu,
kama itakavyohitajika na mamlaka yoyote au kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sheria ya Usimamizi wa Vinasaba vya Binadamu, Kuzuia na kudhibiti Matumizi ya Dawa za kulevyta na sheria nyingine yoyote.
(3) Bila kuathiri huduma zilizotajwa katika kifungu kidogo cha (1), maabara ya sayansi jinai na Vinasaba inaweza kufanya uchunguzi wa sampuli nyingine zisizohusiana na madai pale inapohitajika.
- Sura 20, 73 na 95
- (b) *Huduma za maabara ya ubora wa bidhaa*
- Huduma za maabara ya ubora wa bidhaa
- 21.**-(1) Itakuwepo ndani ya Mamlaka maabara inayoshughulikia masuala ya huduma za ubora wa bidhaa.
(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Mamlaka itafanya uchunguzi wa-.
(a) chakula, dawa, vipodozi, pamoja na malighafi zinazohusika;
(b) kimaikrobaiolojia;
(c) kutumia mitambo; na
(d) uchunguzi wa dawa asilia.
(3) Mamlaka inaweza kutoa huduma nyingine zitakazotolewa na maabara ya ubora wa bidhaa kwa kadri ambavyo itahitajika.
- Sura 219
- (c) *Huduma za maabara za usimamizi wa kemikali*
- Huduma za maabara za usimamizi wa kemikali
- 22.**-(1) Itakuwepo maabara ndani ya Mamlaka inayoshughulikia masuala ya huduma za usimamizi wa kemikali.
(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Mamlaka utafanya uchunguzi wa-
(a) kemikali, bidhaa za kemikali na malighafi kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani;
(b) sampuli zinazohusiana na afya mahali pa kazi kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Usalama Kazini na
- Sura 182
- Sura 297 na 191

uchafuzi wa mazingira kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Mazingira; na

- (c) huduma nyingine kadri itakavyohitajika.

Ukomo wa
ripoti ya
uchunguzi

23. Ripoti ya matokeo ya uchunguzi wa kimaabara itatolewa na Mamlaka kuhusu huduma za uchunguzi wa sayansi jinai, ubora wa bidhaa na usimamizi wa kemikali na uamuvi huo utakuwa ni wa mwisho.

**SEHEMU YA SITA
USIMAMIZI WA MAABARA**

(a) *Usajili wa maabara*

Usajili wa
maabara

24.-(1) Maabara haitaruhusiwa kutoa huduma za maabara za kemia, sayansi jinai na Vinasaba zinazosimamiwa chini ya Sheria hii isipokuwa kama maabara hiyo imesajiliwa chini ya Sheria hii.

(2) Maabara haitasajiliwa isipokuwa kama ina watumishi walio na sifa zinazofaa na eneo la maabara lina vifaa vinavyokidhi viwango vilivyoainishwa kwenye kanuni.

(3) Maombi ya usajili yatakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria hii na yataambatana na tozo iliyoainishwa kwenye kanuni.

(4) Mkemia Mkuu wa Serikali ataweka na kutunza rejestra ya maabara ambayo ndani yake taarifa na maelezo ya maabara zilizosajiliwa zitaingizwa.

(5) Mtu atakayekiuka kifungu hiki anatenda kosa na atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu au vyote.

Utoaji wa
cheti

25.-(1) Kemikali iliyoajiliwa, mfanyakishara wa kemikali aliyesajiliwa, maabara ya kutoa mafunzo, maabara ya kemia, sayansi jinai na Vinasaba iliyoajiliwa itapewa cheti.

(2) Utaratibu wa kusajiliwa na utoaji wa cheti uliotolewa chini ya Sheria hii utakuwa kama utakavyoainishwa katika Kanuni.

Kufutwa kwa
usajili wa
maabara

26.-(1) Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ridhaa ya Bodi, anaweza kufuta usajili wa maabara yoyote ya kemia, sayansi jinai na Vinasaba iwapo-

-
- (a) cheti cha usajili kimepatikana kinyume na masharti ya Sheria hii; au
(b) uendeshaji wa maabara unakiuka masharti yoyote yaliyoambatana na usajili.
(2) Bodi, kabla ya kufuta usajili wa maabara, chini ya Sheria hii atampa nafasi mmiliki wa maabara hiyo nafasi ya kusikilizwa.
(3) Ufutaji wowote wa usajili wa maabara uliofanywa chini ya kifungu hiki utachapishwa kwenye *Gazeti* la Serikali.

Kukata rufaa

- 27.**-(1) Mtu ambaye hataridhishwa na uamuzi ya Bodi, anaweza ndani ya kipindi cha miezi mitatu, baada ya tarehe ya kutolewa uamuzi kukata rufaa kwa Waziri.
(2) Waziri ndani ya mwezi mmoja baada ya kufanya uamuzi ataruhusu rufaa yoyote, kubadilisha au kurekebisha uamuzi wa Bodi na kutoa amri kadri atavyoona inafaa.
(3) Waziri ndani ya mwezi mmoja baada ya kutoa maamuzi ya rufaa, atatoa nakala ya uamuzi kwa mwombaji.

Taarifa ya kufunga au kubadilisha umiliki

- 28.**-(1) Mmiliki wa maabara ambaye anataka kufunga maabara au kubadilisha umiliki wa maabara atamtaarifu Mkemia Mkuu wa Serikali, miezi mitatu kabla ya kufunga au ubadilisha umiliki wa maabara.
(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1) mmiliki ndani ya miezi mitatu kabla ya kufunga maabara, atatakiwa kuwasilisha programu ya kufunga maabara kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kama ilivyoinishwa katika kanuni kwa ajili ya kuidhinisha, kusimamia na kukagua.
(3) Mtu ambaye atashindwa kutoa taarifa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali juu ya kufunga maabara au ubadilishaji umiliki, anatenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

(b) Ukaguzi wa maabara

Ukaguzi wa maabara

- 29.**-(1) Bodi inaweza kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa matakwa ya masharti ya sheria hii yanafuatwa, itafanya au kupelekea kufanywa ukaguzi katika eneo au huduma yoyote.
(2) Waziri, baada ya kushauriwa na Bodi, atatengezeza Kanuni zitakazoainisha-

-
- (a) uteuzi, mamlaka na sifa za wakaguzi; na
 - (b) kufanya ukaguzi kwa madhumuni ya sheria hii.

(c) *Utunzaji Kumbukumbu na Utoaji wa Taaarifa*

Utunzaji wa
kumbukumbu

30. Mmiliki au mwendeshaji wa Maabara atatunza kumbukumbu au huduma zinazotolewa, mapendekezo kutokana na ukaguzi uliopita, na hatua zilizochukuliwa kama zipo.

Utoaji wa
taarifa

31.-(1) Mmiliki au mwendeshaji wa maabara iliyosajiliwa atawasilisha taarifa kwa Msajili mara mbili kwa mwaka kwa namna iliyoinishwa kwenye kanuni.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), mtu yoyote atakayeshindwa kuwasilisha ripoti, cheti chake au kibali kitafutwa au kusimamishwa.

SEHEMU YA SABA
KANZIDATA YA TAIFA YA VINASABA VYA BINADAMU

Kanzidata ya
Taifa ya
Vinasaba vya
Binadamu
Sura ya 73

32.-(1) Itakuwepo ndani ya Mamlaka, Kanzidata ya Taifa ya Vinasaba vya Binadamu, ambayo itakuwa ni hifadhi kuu ya kumbukumbu ya Vinasaba vya binadamu.

(2) Zitakuwepo maabara teule za vinasaba vya binadamu kama ilivyoainishwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Vinasaba vya binadamu.

(3) Kila maabara teule ya vinasaba vya binadamu itawasilisha taarifa za vinasaba kwa Mamlaka.

(4) Taarifa zitakazowasilishwa kwa Mamlaka, zitajumuisha taarifa kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tano la Sheria hii.

(5) Bodi inaweza, kufanya mapitio ya orodha ya taarifa zilizopo kwenye Kanzidata.

Fursa ya
kupata taarifa

33.-(1) Mkemia Mkuu wa Serikali kwa tozo au bila tozo ataidhinisha kutolewa kwa taarifa zilizomo kwenye kanzidata kwa kutuma maombi ya maandishi kuhusu masuala yaliyoainishwa kwenye kanuni.

(2) Taarifa ilizomo kwenye Kanzidata ya Taifa ya Vinasaba vya Binadamu inaweza kutolewa kwa-

- (a) mtu yeyote ambaye Mkemia Mkuu wa Serikali atamuidhinisha; au

(b) taasisi za Serikali, wakala, na idara nyingine.

(3) Mtu yeoyote, aliyepata, anayetua au kuchapisha taarifa zilizomo kwenye Kanzidata bila ya idhini ya maandishi kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali anatenda kosa na akipatikana na hatia, atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote.

SEHEMU YA NANE

KITUO CHA TAIFA CHA KUTHIBITI MATUKIO YA SUMU

Kituo cha
Taifa cha
kuthibiti
matukio ya
sumu

34.-(1) Kituo cha Taifa cha kuthibiti na kusimamia matukio ya sumu, kitaanzishwa na kusimamiwa na Mamlaka.

(2) Mamlaka itaratibu na kusimamia matukio ya sumu.

(3) Maabara za Kanda za Mamlaka, zitakuwa vituo vidogo kwa Kituo cha Taifa cha Kuthibiti na Kusimamia Matukio ya sumu.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Kituo cha Taifa cha kuratibu matukio ya sumu kitakeleza majukumu yafuatayo:

(a) kutoa taarifa kwa umma kuhusiana na sumu;

(b) kufanya uchunguzi wa kimaabara wa sumu;

(c) kukusanya taarifa kutoka katika vituo vya kukusanya taarifa juu ya uchunguzi wa magonjwa na matukio ya sumu;

(d) kutoa mafunzo na utafiti wa masuala ya sumu; na

(e) kutunza kumbukumbu za matukio ya sumu na taarifa za kisayansi kuhusiana na sumu.

Uteuzi wa
vituo vya
utoaji taarifa

35.-(1) Mamlaka itateua vituo vya utoaji taarifa vya afya na taasisi nyingine kuwa vituo vidogo vya kutoa taarifa ambazo zitatoa taarifa za matukio ya sumu.

(2) Kila kituo kidogo kilichoteuliwa kwa ajili ya kutoa taarifa za matukio ya sumu kitawasilisha taarifa za matukio ya sumu kwa Mamlaka.

(3) Taratibu na shughuli za vituo vya utoaji taarifa za matukio ya sumu zitakuwa kama zilivyoainishwa kwenye kanuni.

SEHEMU YA TISA MASUALA YA FEDHA

Vyanzo vya mapato	<p>36.-(1) Vyanzo vya mapato vya Mamlaka vitajumuisha-</p> <ul style="list-style-type: none">(a) fedha zitakazotengwa na Bunge;(b) fedha au mali zinazoweza kumilikiwa au kupatikana kutokana na vyanzo vingine;(c) ada zilizowekwa na tozo zilizopatikana kutokana na huduma zilizotolewa;(d) mapato yatokanayo na kuuza rasilimali au vyanzo vingine vya mapato vilivyoainishwa na mamlaka;(e) zawadi, misaada na michango; na(f) fedha nyingine zozote zitakazokopwa, kupokelewa au kupatikana kwenye Mamlaka kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. <p>(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), Serikali kila mwezi katika kipindi cha mwaka wa fedha kutoa kwenye Mamlaka kiasi cha fedha zilizotolewa na Bunge kugharamia matumizi ya shughuli za Mamlaka.</p> <p>(3) Ada na tozo zitaainishwa kwenye Kanuni.</p> <p>(4) Kwa madhumuni ya vifungu vidogo vya (1) na (2), ada na tozo zilizowekwa kwa huduma zinazotolewa kuhusiana na sampuli au vielelezo vilivyowasilishwa kwa ajili ya masuala yanayohusu jinai, maafa, ulinzi na usalama na sampuli nyingine zozote zenyet maslahi ya Taifa zitagharimiwa na Serikali kupitia fungu maalumu litakaloanzishwa chini ya Mamlaka.</p>
Makadirio ya mapato na matumizi	<p>37.-(1) Mkemia Mkuu wa Serikali atatayarisha na kuwasilisha kwenye Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa makadirio ya mapato na matumizi ya Mamlaka miezi mitatu kabla ya mwisho wa mwaka unaofuata.</p> <p>(2) Bodi itapeleka kwa Waziri makadirio ya mapato na matumizi yaliyoandaliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa ajili ya kuidhinishwa.</p> <p>(3) Hakuna matumizi yatakayofanywa nje ya bajeti ya Mamlaka isipokuwa kama matumizi hayo yataidhinishwa na Waziri chini ya kifungu kidogo cha (2).</p>
Bajeti ya nyongeza	<p>38.-(1) Iwapo, katika mwaka wowote wa fedha, Mamlaka inahitaji kufanya matumizi yoyote ambayo hayakuainishwa kwenye bajeti, au yanayozidi kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika bajeti ya mwaka huo wa fedha, Bodi itaidhinisha bajeti ya nyongeza kwa madhumuni ya matumizi hayo.</p>

(2) Bajeti ya mwaka na kila bajeti ya nyongeza itakuwa katika utaratibu na itajumuisha taarifa kadri Bodi atakavyoelekeza.

Uwasilishaji
wa taarifa ya
fedha ya
mwaka

39.-(1) Katika Sheria hii “mwaka wa fedha” unamaanisha mwaka wa fedha wa Serikali.

(2) Mkemia Mkuu wa Serikali kila mwisho wa mwaka wa fedha ataandaa taarifa ya utekelezaji ya mwaka ya shughuli zilizofanyika katika mwaka wa fedha na kuwasilisha taarifa hiyo kwa Bodi.

(3) Mkemia Mkuu wa Serikali atahakikisha taarifa ya fedha ya mwaka imeandalowi na kukaguliwa na Mkguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mwakilishi wake ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya mwaka wa fedha.

(4) Taarifa ya fedha zitajumuisha-

- (a) taarifa ya utendaji wa kifedha;
- (b) taarifa ya hali ya kifedha;
- (c) taarifa ya mtiririko wa mapato na matumizi;
- (d) taarifa ya mabadiliko ya faida au hasara; na
- (e) maelezo ya ufanuzi wa taarifa za fedha.

Uwasilishwaji
wa taarifa ya
fedha ya
mwaka

40.-(1) Mkemia Mkuu wa Serikali atawasilisha kwa Waziri nakala za taarifa za hesabu zilizokaguliwa miezi mitatu kila baada ya mwisho wa mwaka wa fedha.

(2) Waziri atawasilisha nakala ya taarifa ya fedha ya Mamlaka Bungeni, ndani ya miezi miwili au katika kikao kinachofuata cha bunge, baada ya kupata ripoti.

Usimamizi na
udhibiti wa
fedha

41.-(1) Mamlaka itatunza vitabu vya fedha na kuhifadhi kumbukumbu za uendeshaji wake kwa mujibu wa viwango vya kihasibu vya kitaifa.

(2) Mamlaka itaandaa na utuzwaji vitabu vya fedha sahihi na kumbukumbu zinazohusu-

- (a) mali na madeni;
- (b) stakabadhi za matumizi ya fedha na matumizi mengineyo ya fedha; na
- (c) taarifa ya hali ya kifedha pamoja na taarifa inayoonesha hali ya utendaji wa kifedha itakayoandalowi katika kila mwaka wa fedha.

(3) Fedha na rasilimali za Mamlaka zitatumika kwa madhumuni yaliyowekwa chini ya Sheria hii.

(4) Matumizi ya fedha za Mamlaka yatatakiwa kufuatiliwa na kupitiwa na Bodi.

Misingi ya
uendeshaji

42.-(1) Mamlaka-

- (a) itafungua na kuendesha vitabu vyote vya fedha, leja, jarida na vitabu vingine vya ziada vya fedha kulingana na miongozo ya kihasibu; na
- (b) itapitia na kubadili nyaraka zake ili kuwezesha utunzaji sahihi wa vitabu vya fedha kama itakavyoelekezwa na mamlaka husika.

(2) Fedha zote zilizopokelewa zitawekwa katika akaunti ya makusanyo ya mapato na malipo yatafanyika katika akaunti ya matumizi.

Mamlaka ya
kuwekeza

43. Kwa mujibu wa idhini ya Msajili wa Hazina na Waziri, Mamlaka inaweza kuwekeza fedha kwa namna itakavyoona inafaa.

**SEHEMU YA KUMI
MASHARTI MBALIMBALI**

Mamlaka ya
Waziri
kutunga
kanuni

44. Waziri, anaweza kutunga kanuni kuhusiana na-

- (a) uchukuaji wa sampuli na uwasilishaji wa sampuli za sayansi jinai;
- (b) viwango vya majengo, vifaa pamoja na sifa za watumishi wa maabara za kemia, sayansi jinai na vinasaba vya binadamu;
- (c) taratibu za usajili na utoaji wa vyeti kwa maabara za kemia, sayansi jinai na Vinasaba vya binadamu;
- (d) aina na taratibu za ukaguzi wa maabara za kemia, sayansi jinai na Vinasaba vya binadamu;
- (e) namna ya uwasilishaji taarifa za maabara za kemia, sayansi jinai na Vinasaba vya binadamu;
- (f) uteuzi, uendeshaji na taratibu za vituo vya kutoa taarifa za matukio ya sumu;
- (g) utunzaji wa kumbukumbu zitokanazo na kazi za Mamlaka;

-
- (h) mamlaka, majukumu, mwenendo, sifa na taratibu za Mchunguzi wa Kimaabara wa Serikali;
 - (i) tozo na ada zingine;
 - (j) uchunguzi wa Vinasaba vy a binadamu na kanzidata; na
 - (k) masuala menginezo yoyote kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

Kinga ya
wajumbe wa
Bodi na
maafisa wa
Mamlaka.

Umiliki wa
raslimali na
madeni
Sura 245 na
Ts.Na.106 la
Mwaka 2000

Uhamisho wa
watumishi na
haki zao.

Sura 245
na Ts.Na.106
la Mwaka
2000

Ujira wa
wajumbe wa
Bodi, kamati
za kitaalamu
na
wafanyakazi

Ustawi na
usalama wa
watumishi

Mgongano wa
kimaslahi

45. Chochote kilichofanywa na Mkemia Mkuu wa Serikali, mjambe yejote wa Bodi, mjambe wa kamati, mwajiriwa au mtu yejote aliyepewa mamlaka ya kutekeleza majukumu chini ya Sheria hii, kama kimefanywa kwa nia njema wakati wa utekelezaji wa majukumu yake au anayotakiwa kufanya kwa mujibu wa Sheria hii, hakitampelekea mjambe au afisa kuwa na hatia kuhusu suala hilo au kitu alichokifanya.

46. Mali zote, haki, majukumu, madeni na rasilimali zinazomilikiwa na Mamlaka kutohana na masharti ya Sheria ya Wakala za Serikali na amri iliyoanzisha Wakala wa Serikali (Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali) ya mwaka 2000, vitaendelea baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii kuendelea kuwa chini ya Mamlaka.

47. Mwajiriwa au mteuliwa wa Mamlaka iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali na Amri iliyoanzisha Wakala wa Serikali (Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali) ya mwaka 2000 baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, ataendelea kuwa mwajiriwa wa Mamlaka katika nafasi aliyokuwa nayo kabla ya Sheria hii haijaanza kutumika.

48. Wajumbe wa Bodi, kamati ya kitaalamu na watumishi watakuwa na stahili ya malipo au posho kama zitakavyoidhinishwa na Waziri, baada ya kushauriwa na Msajili wa Hazina na chombo kingine chochote kinachohusika.

49. Mkemia Mkuu wa Serikali atawajibika kwa ustawi na usalama wa watumishi katika sehemu ya kazi kwa maendeleo ya Mamlaka.

50.-(1) Kila mwajiriwa wa Mamlaka hataruhusiwa kufanya biashara inazosimamiwa na Sheria hii.

(2) Kila mwajiriwa ataepuka kufanya shughuli ambazo zinaweza kukinzana na majukumu yake kama mtumishi wa Mamlaka.

(3) Kila mfanyakazi atakuwa na jukumu la utii kwa mteja na atazuiwa kumwakilisha mtu yoyote mwininge mwenye maslahi kinyume na yale ya mteja au ana majukumu tofauti ambayo yatamzuia mtu huyo kuepuwa upendeleo au kukiuka jukumu la utii.

(4) Kila mfanyakazi atasaini kwa tarehe mgongano wa maslahi ikionyesha uhalisia au mgongano wa maslahi kama ulivyoainishwa kwenye Kanuni.

(5) Pale ambapo ndani ya mwezi mmoja, mwajiriwa atashindwa kusaini kwa tarehe mgongano wa maslahi katika taarifa inayoonyesha uhalisia au mgongano wa maslahi bila kuwa na sababu ya msingi iliyowekwa kisheria, Bodi inaweza kusitisha ajira yake au inaweza kuamua suala0 hilo kwa kadri itakavyoona inafaa.

(6) Fomu zinazopaswa kujazwa na kila mwajiriwa, zitawasilishwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kupitiwa na kuruhusiwa.

Usiri na utoaji
wa taarifa

51.-(1) Kila mwajiriwa au wakala aliyeidhinishwa na Mamlaka, atatakiwa kwa mara zote atakapokuwaa anashughulikia nyaraka yoyote, sampuli au matokeo ya uchunguzi, kuweka usiri.

(2) Mkemia Mkuu wa Serikali, wajumbe wa Bodi, mjumbe wa kamati ya kitaalamu, mwajiriwa wa Mamlaka na wakala aliyeidhinishwa, atatakiwa kuzichukulia kuwa ni siri taarifa yoyote ambayo anaifahamu wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

(3) Masharti ya kifungu hiki yataendelea kutumika kwa watu wote ambao wanahusika na uchunguzi wa sayansi jinai na uchunguzi wa Vinasaba na utoaji matokeo ya maabara kwa kipindi chote cha maisha yao ama au la mtu huyo ameacha kujihusisha au kuajiriwa kwa ajili ya kuendeleza utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

(4) Bila kujali masharti ya Sheria hii, Mkemia Mkuu wa Serikali anaweza kuchapisha au kupelekea kuchapishwa taarifa yoyote iliyotolewa kwa Mamlaka au taarifa yoyote yaliyoko kwenye kumbukumbu au mrejesho yaliyotolewa na Mamlaka kwa mfumo wa muhtasari, ambao hautawezesha utambuzi wa chanzo cha taarifa, kumbukumbu au mrejesho.

(5) Mtu yejote ambaye amekuwa akijihuisha na usimamizi wa Sheria hii na akatoa taarifa yoyote iliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii, kwa mtu yejote kinyume na

masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini isiyopungua milioni tano au kutumikia kifungu kisichopungua miaka mitano au vyote viwili kwa pamoja.

Mamlaka ya
Waziri kutoa
maelekezo

Makosa ya
yanayohusu
kuharibu,
kubadilisha
nyaraka au
taarifa

Wajibu wa
kisheria wa
kampuni na
wabia wake

Mamlaka ya
kufilisha
kosa

Adhabu za
jumla

52. Waziri anaweza, kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, kutoa maelekezo kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji na utendaji wa Mamlaka na Sheria hii.

53. Mfanyakazi yoyote wa mamlaka ambaye kwa kujuu au makusudi anaharibu au anabadilisha nyaraka au ripoti ya utafiti wa kimaabara wakati wa kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii anatenda kosa.

54.-(1) Pale ambapo kosa limetendwa na kampuni au mbia, kila mkurugenzi, mtendaji mkuu, au afisa wa shirika au mbia au afisa wa ubia ambaye alikuwa na ufahamu au alipaswa kuwa na ufahamu wa kutendeka kwa kosa atakuwa na hatia ya kosa.

(2) Mtu ye yoyote atawajibika yeye mwenyewe kwa kosa alilolitenda kinyume na Sheria hii, iwe amelifanya yeye au kama wakala au mtumishi wa mtu.

55.-(1) Mamlaka inaweza, ikiwa imejiridhisha kuwa mtu huyo ametenda kosa chini ya Sheria hii, itafifisha kosa kwa kumkubalia mtu huyo kulipa kiasi cha fedha kisichozidi shilingi milioni tano.

(2) Mamlaka iliyotolewa chini ya kifungu hiki, yatatumika pale ambapo mtu atakiri kwamba ametenda kosa chini ya Sheria hii.

(3) Kiasi chochote cha fedha kitakachopokelewa chini ya kifungu hiki kitachukuliwa kama vile ni kiasi cha fedha kilichotozwa na mahakama kwa kosa hilo.

56. Mtu ye yoyote atakayetenda kosa kinyume na Sheria hii ambapo adhabu haijaainishwa popote, atawajibika kulipa faini-

(a) isiyopungua shilingi milioni moja ikiwa anayetenda kosa ni mtu binafsi au kifungo kisichopungua miezi sita au vyote kwa pamoja; na

(b) isiyopungua shilingi milioni tano ikiwa aliyetenda kosa ni kampuni.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 7)

UTARATIBU, MUDA, UKOMO NA UENDESHAJI WA VIKAO VYA BODI

Muda wa
Bodi

1.-(1) Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi watashika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya uteuzi na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

(2) Kwa mjambe ambaye ameteuliwa kutokana na kushika madaraka katika ofisi yake, atakoma kuwa mjambe mara atakapoacha kushika madaraka katika ofisi hiyo.

(3) Mjambe wa Bodi atakoma kuwa mjambe kama-

- (a) atafariki au kijiuzuru kwa sababu zozote zile;
- (b) atashindwa kuhudhuria vikao vitatu vya Bodi mfululizo bila sababu za msingi;
- (c) amehukumiwa kwa makosa ya jinai kwa zaidi ya miezi sita; au
- (d) atapata ugonjwa wa akili.

(4) Pale mjambe aliyeuleliwa atakoma kuwa mjambe kwa sababu zilizoainishwa kwenye kifungu kidogo cha (3), Waziri atateua mtu mwingine kuziba nafasi yake na mtu aliyeuleliwa kuwa mjambe kwa kipindi kilichobakia cha mjambe wa awali.

Vikao vya
Bodi

2.-(1) Bodi itaanya kikao angalau kimoja kila baada ya miezi mitatu katika muda na sehemu kadiri itakavyoonekana inafaa ili kuendesha shughuli zake.

(2) Bila kujali kifungu cha (1), Mwenyekiti anaweza, baada ya kupata idhini ya theluthi mbili ya wajumbe kuitisha kikao cha dharura kujadili suala linalohitaji uamuzi wa haraka.

(3) Pale Mwenyekiti anapokuwa hayupo, wajumbe watakaokuwepo kwenye kikao, watachagua mmoja wa wajumbe kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho na mjambe huyo aliyechaguliwa atakuwa na wajibu wa kutoa taarifa ya kikao hicho kwa Mwenyekiti.

(4) Bodi itahakikisha muhutasari wa vikao vyote vilivyofanyika inaandikwa na kuhifadhiwa, na muhutasari wa kila kikao cha Bodi utasomwa na kuthibitishwa au kurekebishwa katika kikao cha Bodi kitakachofuata na kutiwa saini na Mwenyekiti na Katibu.

Akidi

3.-(1) Akidi katika kikao chochote cha Bodi itakuwa ni theluthi mbili ya wajumbe.

(2) Masuala yaliyopendekezwa katika kikao cha Bodi, yataamuliwa na idadi kubwa ya kura za wajumbe waliohudhuria.

(3) Uhalali wa taarifa yoyote ya kikao cha Bodi iliyoundwa kihalali hautaathiriwa na kukosekana kwa mjambe ye yoyote asiyehudhuria au kwa kasoro itakayotolewa na mjambe asiyehudhuria kikao.

The Government Chemist Laboratory Authority Act

- | | |
|--------------------------------|---|
| Maelekezo ya
Bodi | 4. Maagizo, maelekezo, matangazo au hati iliyotayarishwa au kutolewa kwa niaba ya Bodî inatakiwa kutiwa saini na Mwenyekiti au Katibu. |
| Udhibiti wa
masuala
yake | 5. Bodî itakuwa na mamlaka ya kujipangia kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli zake. |
| Ushahidi wa
Nyaraka | 6. Nyaraka yoyote inayosainiwa na Mwenyekiti au Katibu kutokana na azimio la Bodî zitapokelewa katika mahakama au mabaraza au vyombo vingine vilivyoidhinishwa kupokea ushahidi na zitakuwa, isipokuwa kama itathibitika vinginevyo, ushahidi wa kutosha wa kile kitakachokuwa katika nyaraka. |

JEDWALI LA PILI

**UTEUZI, MUUNDO, KIPINDI CHA KAMATI NA TARATIBU ZA VIKAO VYA
KAMATI YA KITAALAMU YA SAYANSI JINAI**

(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 9)

Uteuzi wa
Wajumbe wa
Kamati

1.-(1) Waziri atateua Mwenyekiti na wajumbe wengine sita wa Kamati ya Kitaalamu ya Sayansi Jinai kama ifuatavyo:

- (a) mwakilishi kutoka Ofisi ya Uchunguzi wa Makosa ya Jinai katika Jeshi la Polisi;
- (b) mwakilishi kutoka Idara ya Baiokemia ya chuo kikuu kinachotambulika nchini;
- (c) daktari bingwa wa sayansi jinai kutoka taasisi ya umma;
- (d) mwakilishi kutoka Tume ya Kudhibiti dawa za Kulevy;
- (e) afisa wa Sheria atakayependekezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na
- (f) mwakilishi kutoka Idara ya Wanyamapori chini ya Wizara husika.

(2) Mkurugenzi anayehusika na masuala yanayohusu huduma ya Sayansi Jinai na Vinasaba atakuwa katibu wa kamati.

(3) Kamati inaweza, iwapo itaona inafaa, kumualika mtu ye yote kutoa ushauri wa kitaalam wakati wa mikutano yake, isipokuwa mjumbe huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura na ujumbe wake utakoma baada ya suala husika kukamilika.

Majukumu ya
kamati

2. Majukumu ya kamati, yatakuwa ni kumshauri Mkemia Mkuu wa Serikali kwenye masuala yote yanayohusiana na huduma za sayansi jinai.

Muda wa kuaa
madarakani

3.-(1) Mwenyekiti na wajumbe wa kamati watashika nyazifa zao kwa kipindi cha miaka mitatu na watakuwa na sifa za kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja, isipokuwa pale uteuzi wao utakapokuwa umesitishwa na Waziri, au ujumbe wao utakuwa umesitishwa kwa sababu zozote zile.

(2) Kwa mjumbe ambaye ameteuliwa kutokana na kushika madaraka katika ofisi yake, atakoma kuwa mjumbe mara atakapoacha kushika madaraka katika ofisi hiyo.

- (3) Mjumbe wa kamati atakoma kuwa mjumbe kama-
- (a) atafariki au kuijuzuru kwa sababu zozote zile;
- (b) atashindwa kuhudhuria vikao vitatu vya kamati mfululizo bila sababu za msingi;
- (c) atahukumiwa kwa makosa ya jinai kwa zaidi ya miezi sita; au
- (d) atapata ugonjwa wa akili.

(4) Pale mjumbe aliyeuleliwa atakoma kuwa mjumbe kwa sababu yoyote ile, Waziri atateua mtu mwingine kuziba nafasi yake na mtu aliyeuleliwa atakuwa mjumbe kwa kipindi kilichobakia cha mjumbe wa awali.

Vikao vya
Kamati

- 4.**-(1) Kamati itafanya kikao angalau kimoja kila baada ya miezi mitatu katika muda na sehemu kadiri itakavyoonekana inafaa ili kuendesha shughuli zake.
(2) Mwenyekiti anaweza, baada ya kupata idhini ya theluthi mbili ya wajumbe kuitisha kikao cha dharura kujadili suala linalohitaji uamuzi wa haraka.
(3) Pale Mwenyekiti anapokuwa hayupo, wajumbe watakaokuwepo kwenye kikao, watachagua mmoja wa wajumbe kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho.
(4) Kamati itahakikisha muhutasari wa vikao vyote vilivyofanyika inaandikwa na kuhifadhiwa, na muhutasari wa kila kikao cha kamati utasomwa na kuthibitishwa au kurekebishwa katika kikao cha kamati kitakachofuata na kutiwa saini na Mwenyekiti na Katibu.

Akidi

- 5.**-(1) Akidi katika kikao chochote cha kamati itakuwa ni theluthi mbili ya wajumbe.
(2) Masuala yaliyopendekezwa katika kikao cha kamati, yataamuliwa na idadi kubwa ya kura za wajumbe waliohudhuria.
(3) Uhalali wa taarifa yoyote ya kikao cha kamati iliyoundwa kihalali hautaathiriwa na kukosekana kwa mjumbe ye yoyote asiyehudhuria au kwa kasoro itakayotolewa na mjumbe asiyehudhuria kikao.

Mwenendo

- 6.** Kwa mujibu wa Jedwali hili, **kamati itajipangia kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli zake.**

JEDWALI LA TATU

**MUUNDO, UTEUZI, KAZI NA TARATIBU ZA KAMATI YA KURATIBU
MATUKIO YA SUMU**

(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 12)

Uteuzi wa
Wajumbe wa
Kamati na
Muundo

1. Waziri atateua **Mwenyekiti na** wajumbe **wengine sita** wa Kamati ya Kuratibu matukio ya Sumu kama ifuatavyo:

- (a) mwakilishi kutoka Wizara ya Kilimo;
- (b) mwakilishi kutoka Ofisi ya Uchunguzi wa Makosa ya Jinai katika Jeshi la Polisi;
- (c) mwakilishi Mwandamizi kutoka kitengo cha Ubora, Hospitali ya Taifa Muhimbili;
- (d) mwakilishi kutoka Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu;
- (e) mwakilishi kutoka Idara ya Kinga, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; na
- (f) mwakilishi kutoka Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu.

(2) Mkurugenzi anayehusika na masuala yanayohusiana na huduma ya Sayansi Jinai na Vinasaba atakuwa katibu wa kamati.

(3) Kamati inaweza, iwapo itaona inafaa, kumualika mtu ye yote kutoa ushauri wa kitaalam wakati wa mikutano yake, isipokuwa mjambe huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura na ujumbe wake utakoma baada ya suala husika kukamilika.

Majukumu ya
kamati

3. Kazi za kamati zitakuwa ni-

- (a) kumshauri Mkemia Mkuu wa Serikali katika masuala ya kitaalamu na kiutawala yanayohusu udhibiti wa sumu;
- (b) kushauri na kuwezesha ushirikiano wa Kitaifa, kikanda na kimataifa aina ya vituo vinavyodhibiti sumu;
- (c) kushauriana kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kushirikiana katika udhibiti wa sumu mpango;
- (d) kushauri kuhusiana na uchukuaji na ukusanyaji wa taarifa, uchunguzi, utoaji taarifa na usambazaji wa taarifa zahusozo madhara ya sumu.

Kipindi cha
Kamati

4.-1) Mwenyekiti na wajumbe wa kamati watashika nyazifa zao kwa kipindi cha miaka mitatu na watakuwa na sifa za kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja, isipokuwa pale uteuzi wao utakapokuwa umesitishwa na Waziri, au ujumbe wao utakuwa umesitishwa kwa sababu zozote zile.

(2) Kwa mjambe ambaye ameteuliwa kutokana na kushika madaraka katika ofisi yake, atakoma kuwa mjambe mara atakapoacha kushika madaraka katika ofisi hiyo.

- (3) Mjambe wa kamati atakoma kuwa mjambe kama-
- (a) atafariki au kujuzuru kwa sababu zozote zile;
- (b) atashindwa kuhudhuria vikao vitatu vya kamati mfululizo bila sababu za

The Government Chemist Laboratory Authority Act

msingi;

- (c) amehukumiwa kwa makosa ya jinai kwa zaidi ya miezi sita; au
(d) atapata ugonjwa wa akili.

(4) Pale mjambe aliyeteuliwa atakoma kuwa mjambe kwa sababu yoyote ile, Waziri atateua mtu mwagine kushika nafasi yake na mtu aliyeteuliwa atakuwa mjambe kwa kipindi kilichobakia cha mjambe wa awali.

Vikao vya
Kamati

5.-(1) Kamati itafanya kikao angalau kimoja kila baada ya miezi mitatu katika muda na sehemu kadiri itakavyoonekana inafaa ili kuendesha shughuli zake.

(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), Mwenyekiti anaweza, baada ya kupata idhini ya theluthi mbili ya wajumbe kuitisha kikao cha dharura kujadili suala linalohitaji uamuza wa haraka.

(3) Pale Mwenyekiti anapokuwa hayupo, wajumbe watakaokuwepo kwenye kikao, watachagua mmoja wa wajumbe kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho.

(4) Kamati itahakikisha muhutasari wa vikao vyote vilivyofanyika inaanidikwa na kuhifadhiwa, na muhutasari wa kila kikao cha kamati utasomwa na kuthibitishwa au kurekebishwa katika kikao cha kamati kitakachofuata na kutiwa saini na Mwenyekiti na Katibu.

Akidi

6.-(1) Akidi katika kikao chochote cha kamati itakuwa ni theluthi mbili ya wajumbe.

(2) Masuala yaliyopendekezwa katika kikao cha Kamati, yataamuliwa na idadi kubwa ya kura za wajumbe waliohudhuria.

(3) Uhalali wa taarifa yoyote ya kikao cha Kamati iliyoendwa kihalali hautaathiriwa na kukosekana kwa mjambe ye yoyote asiyehudhuria au kwa kasoro itakayotolewa na mjambe asihudhuria kikao.

Udhibiti wa
masuala yake

7. Kwa kuzingatia Jedwali hili, Kamati itajipangia kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli zake.

JEDWALI LA NNE

MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

S.L.P. 164 DAR ES SALAAM

MAOMBI YA KUSAJILI MAABARA

(Limetengenezwa chini ya kifungu 24)

1. Mahitaji ya Mwombaji:

- 1.1 Jina:
1.2 Anwani:
1.3 Simu:
1.4 Nukushi:
1.5. Barua pepe:
1.6 Namba ya Usajili wa Kampuni:
1.7 Leseni ya Biashara:

2. Anwani ya Makazi:

- 2.1 Kiwanja No:
2.2 Barabara
2.3 Wilaya:
2.4 Mkoa:

3. Mwombaji (kama tofauti na awali)

- 3.1 Jina:
3.2 Anwani:
3.3 Simu:
3.4 Nukushi:
3.5 Barua pepe:

4. Masharti ya Usajili

- 4.1 Sifa za wataalamu wa Maabara.....
(Ambatanisha vyeti)
4.2 Aina ya maabara (kemia, sayansi jinai au vinasaba, weka alama inavyohitajika)

The Government Chemist Laboratory Authority Act

4.3 Ambatanisha nyaraka zifuatazo:

- (a) Mpango wa Usalama Kazini
- (b) Mpango wa kukabiliana na matukio ya dharura.

Mimi.....natamka kuwa taarifa nilizozitoa hapo juu ni sahihi kwa uelewa wangu.

Sahihi:.....Tarehe:.....

Kwa Matumizi ya Ofisi:

A. Na.:Jina:.....Sahihi:.....Tarehe:.....

JEDWALI LA TANO

TAARIFA ZITAKAZOWEKWA KWENYE KANZIDATA YA VINASABA

(Lmetengenezwa chini ya Kifungu cha 32)

Kanzidata itakuwa na taarifa zitakahusu:

- (1) Matukio ya uhalifu.
- (2) Watoto waliozaliwa.
- (3) Madai.
- (4) Watuhumiwa wa jinai.
- (5) Mahabusu.
- (6) Wafungwa.
- (7) Wafanya fujo.
- (8) Wahalifu wa makosa ya kijinsia.
- (9) Wahanga wa majanga.
- (10) Watuhumiwa au wahalifu wasiohusika.
- (11) Taarifa kuhusina na vitambulisho vya Taifa.
- (12) Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Polisi.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Sheria inayopendekezwa itachangia katika juhudzi za Serikali katika kuboresha ustawi na mazingira ya wananchi wake. Hatua hii inatokana na kuwepo kwa baadhi ya mambo yanayoathiri utendaji kazi wa Mamlaka ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika juhudzi za kufikia malengo na kutimiza majukumu yake.

Mamlaka umekuwa ukitekeleza kazi zake kutokana na mamlaka yanayosimamiwa na sheria nyingine. Hivyo, kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kutatoa mwongozo wa kisheria kuhusiana

na majukumu ya Mamlaka ya serikali, taasisi mbalimbali za umma kwa ujumla. Hatua hii itapunguza migongano na kuongeza uelewa wa wadau juu ya mamlaka na majukumu ya Mamlaka. Kwa nyongeza Sheria inayopendekezwa inaipa mamlaka Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa maabara ya rufaa kwenye masuala yanayohusiana na sayansi jinai na vinasaba, ubora wa bidhaa, usimamizi wa kemikali, uratibu na usimamizi kituo cha matukio ya sumu.

Sheria ya mamlaka inayopendekezwa, inalenga kuanzisha Mamlaka kwa kuainisha majukumu na mamlaka ya kusimamia maabara za kemia, sayansi, jinai na unasaba nchini.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu kuu Kumi.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inapendekeza masharti ya awali ambayo yanajumuisha jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa, pamoja na tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada hii.

Sehemu ya Pili inahusu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, majukumu na mamlaka yake.

Sehemu ya Tatu inahusu masuala ya utawala na mpangilio wa kitaasisi. Sehemu hii inaainisha masharti juu ya uteuzi, majukumu na mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Pia, Sehemu hii inaanzisha kamati mbalimbali za kitaalamu kwa madhumuni ya kumshauri Mkemia Mkuu wa Serikali kwenye masuala yanayohusiana na sayansi jinai na udhibiti wa sumu. Sehemu hii pia inaainisha taratibu za uteuzi wa Mchunguzi wa Serikali na Mkaguzi pamoja na majukumu na mamlaka yao.

Sehemu ya Nne inahusu usimamizi wa sampuli na matokeo ya uchunguzi na matokeo ya kisheria kwa mtu anayetumia cheti cha uchunguzi kilichotolewa chini ya Sheria hii kwa ajili ya kujitangaza bila ya kuwa na idhini ya kimaandishi kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali. Sehemu hii pia inaweka masharti kwenye ripoti za uchunguzi, utoaji wa ripoti, utaratibu na ukubaliwaji wa ripoti hiyo.

Sehemu ya Tano inahusu uanzishaji wa maabara na huduma zinazotolewa na Mamlaka kwa Serikali, sekta binafsi na umma. Maabara hizi zinataka kutoa huduma za Sayansi Jinai (toksikolojia, kemia na dawa za kulevy, biolojia na vinasaba); maabara ya ubora wa bidhaa (vyakula na dawa, kimaikrobiolojia na uchunguzi wa kutumia mitambo) na usimamizi wa kemikali (maabara za

mazingira, uchukuaji wa sampuli za afya mahala pa kazi, kemia na bidhaa za kemia).

Sehemu ya Sita inaipa uwezo Mamlaka ya usimamizi maabara za kemia, maabara za sayansi jinai na vinasaba nchini. Sehemu hii inataka usajili wa maabara na utoaji wa vyeti. Aidha, Sehemu hii inatoa taratibu za utoaji taarifa ya ufungaji au ubadilishaji wa umiliki na kufutwa kwa usajili wa maabara, ubadilishaji wa umiliki na usajili. Vile vile inaweka masharti ya ukaguzi wa maabara, utunzaji wa kumbukumbu na utoaji wa taarifa.

Sehemu ya Saba inahusu uundwaji wa Kamati ya Taifa ya Kanzidata ya Vinasaba vya Binadamu ambayo itakuwa na wajibu wa kumshauri Mkemia Mkuu wa Serikali katika masuala yanayohusu usimamizi wa Kanzidata. Sehemu hii pia inaweka masharti ya kuweza kupata taarifa zinazohusu vianasaba vya binadamu. Pia inaweka adhabu kwa mtu yoyote ambaye anatoa taarifa na kuzichapisha ambazo zipo kwenye kanzidata.

Sehemu ya Nane inahusu kutambua Mamlaka kama kituo cha kitaifa cha kusimamia na kuratibu matukio ya sumu pamoja na kuainisha majukumu yake. Vile vile inaweka masharti kuhusu taarifa za sumu kwa umma, uchunguzi wa kimaabara, uchunguzi wa magonjwa utambuzi na tiba ya matukio ya sumu na pia kutunza kumbukumbu za matukio ya sumu. Sehemu hii pia inaweka masharti kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kuunda vituo vya kutoa taarifa ya matukio ya sumu.

Sehemu ya Tisa inahusu masuala ya fedha ikiwa ni pamoja na vyanzo vya mapato vya Mamlaka, taarifa za fedha za mwaka na uwasilishaji wake, udhibiti wa fedha, bajeti ya mwaka, misingi ya uendeshaji na mamlaka na kuwekeza.

Sehemu ya Kumi inaweka masharti ya jumla ikijumuisha uwezo Waziri kutunga kanunu, kinga ya wajumbe wa Bodi na maafisa wa Mamlaka, umiliki wa raslimali na madeni, uhamisho wa watumishi na haki zao, malipo ya wajumbe wa Bodi, ustawi na usalama wa watumishi. Masuala mengine yaliyoainishwa ni pamoja na ukataji wa rufaa, wajibu wa kisheria wa kampuni, wabia, wakala, wajiriwa, na wajibu wa Mkemia Mkuu wa Serikali kutoza faini badala ya adhabu.

Dar es Salaam,
10 Mei, 2016

UMMY A. MWALIMU
*Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto*